

Google Duo

Google Ireland Limited (“Google”)

Gordon House, Barrow Street, Dublin 4, Ireland

<https://support.google.com/>

Itaanza Kutumika Tarehe 21 Disemba, 2020

Muhtasari wa Mkataba

- Muhtasari huu wa mkataba unafafanua vipengee vikuu vya huduma tunayoitoa kulingana na matakwa ya sheria ya Umoja wa Ulaya¹.
-
- Dhamira yake ni kukusaidia kulinganisha huduma mbalimbali zinazotolewa.
- Maelezo kamili kuhusu huduma tunazozitoa yanapatikana kwenye hati tofauti.

Huduma

Google Duo ni huduma ya mawasiliano ya video inayotolewa kwenye vifaa na mifumo mbalimbali kupitia kiolesura cha wavuti au programu. Muunganisho wa intaneti unahitajika ili kuwasiliana kupitia Google Duo. Google Duo inatolewa na Google kwa kutumia ustadi na umakini unaofaa, ingawa viwango vya chini zaidi vya ubora wa huduma zinazotolewa havijabainishwa.

Bei

Google Duo inatolewa bila malipo na matumizi yake yanapaswa kutii Sheria na Masharti ya Google (yanayopatikana <https://policies.google.com/terms>).

Muda, usasishaji na utamatishaji

Unaweza kupata na kutumia Google Duo mara tu baada ya kujisajili. Hulazimiki kutumia Google Duo kwa muda fulani uliobainishwa na uko huru kuacha kuitumia wakati wowote.

Vipengele kwa ajili ya watumiaji walio na ulemavu

Unaweza kuwasha kipengele cha manukuu unapotumia Google Duo. Maelezo zaidi yanapatikana <https://support.google.com/duo/answer/7660538?hl=en&co=GENIE.Platform=Android>

Maelezo mengine muhimu

Usaidizi kwa Wateja: Usaidizi kuhusu Google Duo unapatikana <https://support.google.com/>.

Migogoro: Unaweza kupeleka malalamiko kwa mtoa huduma mbadala wa utatuzi wa migogoro aliyerodheshwa <https://ec.europa.eu/consumers/odr/main/?event=main.adr.show2> au mtoa huduma mwingine, kama inavyohitajika na sheria ya nchi yako. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye Sheria na Masharti ya Google.

Matukio ya Usalama: Google ina mpango wa kina wa udhibiti wa matukio wa kila siku, usiku na mchana ili kutambua na kushughulikia matukio ya usalama au ya faragha bila kuchelewa. Google pia inatoa Orodha ya Masuala ya Usalama ya Kukagua ili kukusaidia kudhibiti usalama wako mtandaoni.

Data Binafsi: Ili ujisajili kwenye Google Duo, unahitaji kutoa nambari yako ya simu au anwani yako ya barua pepe (au zote mbili). Sera ya Faragha ya Google (inayopatikana <https://policies.google.com/privacy>) inatoa maelezo zaidi kuhusu data binafsi ambayo Google hukusanya unapotumia Google Duo. Sera ya Faragha ya Google si sehemu ya mkataba kati yako na Google wala si sehemu ya muhtasari huu.

¹ Ibara ya 102(3) ya Agizo (EU) 2018/1972 la Bunge la Ulaya na la Baraza la tarehe 11 Disemba 2018 linalounda Kanuni ya Mawasiliano ya Kielektroniki ya Ulaya (OJ L 321, 17.12.2018, uk. 36).